IDS - University of Dar es Salaam, Tanzania
na
CES - University of Leuven, Belgium

# TASWIRA YA KIJAMII NA KIUCHUMI YA KITONGOJI NYAKATOKE

**Respichius D. MITTI**
**na**
**Thadeus G. RWEYEMAMU**

**Julai, 2000**

## SHUKRANI

Tunaushukuru uongozi wa Mkoa wa Kagera kwa kutupa kibali kufanya utafiti mkoani humu. Pia tunaushukuru uongozi wa wilaya ya Bukoba kwa taarifa maridhawa walizotupa kuhusu wilaya ya Bukoba Vijijini. Msaada tulioupata kutoka kwa Bw. Juvenary Katembo (aliyekuwa Mtendaji wa Kata wakati tulipowasili Rubale) katika kuchagua eneo linalofaa kwa utafiti wetu ulikuwa na umuhimu mkubwa. Tunapenda kutoa shukrani zetu kwa Mzee Leonidas Kamakumbi, ambaye kama kiongozi wa kitongoji, ushirikiano wake ulituwezesha kujenga mahusiano mazuri na wanajumuiya. Uongozi wa kijiji pia ulibariki kuwepo kwetu katika jumuiya hii.

Tunatoa shukrani za dhati kwa wote, wa ndani na nje ya Nyakatoke, ambao taarifa zao ndiyo msingi wa ripoti hii. Majina yao yanatajwa katika sehemu husika ndani ya jarida hili. Tunawashukuru pia watafiti wenzetu, Bw. Obadiah Kyakajumba, Bibi Adelina Rwechungura na Bi Augustina John, ambao walifanya usahili wa dodoso ambazo baadhi ya takwimu zake zimetumika katika ripoti hii. Pia tunamshukuru Bw. Julius Majula aliyeshughulikia uingizaji wa takwimu kwenye kompyuta.

Shukrani za pekee ziwaendee viongozi wa vikundi mbali mbali vya Nyakatoke, waliotupa taarifa za miundo na shughuli za vikundi vyao, orodha yao kamili imetolewa kwenye *kiambatanisho*. Aidha tunawashukuru Bw. Adrian Kaiza, Bw. Lucas Rwabishugi, Bw. Abdulmalik Mushobozi, Bw. Leonidas Kamakumbi na Bw. Paulo Rwegasira, walioupitia mswada na kutoa maoni yao.

Kazi hii isingekamilika bila ya msaada wa Mradi wa Maendeleo ya Jamii Kagera- KCDP, Chuo cha Utafiti wa Kilimo Maruku, BDRDP, Chuo Kikuu cha Bukoba na Ofisi ya Kilimo na Mifugo wilayani, kwa kutuwezesha kupata rejea. Tunamshukuru pia Bw. Joachim De Weerdt kwa kutupa mwongozo na misaada mbali mbali katika utayarishaji wa ripoti hii.

Mwisho, lakini muhimu, tunapenda kuzishukuru familia zetu, ambazo bila ya uvumilivu na ustahimilivu wakati wa vipindi virefu vya kutokuwapo kwetu, shughuli hii isingewezekana.

# YALIYOMO

**Utangulizi**

**1. Jiografia, Udongo na Mvua......................... ........ 1**
1.1. Mahali ilipo...................................................... 1
1.2. Udongo na Mvua............................................. 2

**2. Umilikaji na Utumiaji wa Ardhi.............................. 3**
2.1. Sheria za Umilikaji.......................................... 3
2.2. Matumizi ya Ardhi........................................... 5

**3. Kilimo na Ufugaji................................................ 7**
3.1. Kilimo............................................................... 7
3.2. Mifugo.............................................................. 9

**4. Miundo-mbinu, Masoko na Biashara.................... 10**
4.1. Mawasiliano..................................................... 10
4.2. Elimu............................................................... 11
4.3. Afya................................................................. 13
4.4. Masoko na Biashara........................................ 15
4.5. Nguvukazi........................................................ 16

**5. Historia Fupi ya Nyakatoke................................. 17**
5.1. Makazi ya Awali............................................... 17
5.2. Kukua kwa Nyakatoke...................................... 20
5.3. Muundo wa Makazi.......................................... 22
5.4. Mustakabali wa Jamii...................................... 24

**6. Uhakika wa Jamii katika Kukabiliana na 'Mazingira' (Maisha ya kila Siku)........................................... 26**
6.1. Ushirikiano: Zamani na Sasa.......................... 26
6.2. Muungano na Bujuni........................................ 27
6.3. Vikundi Vingine................................................ 28
6.4. Ushirikiano Nje ya Makundi............................. 30

# ORODHA YA VIELELEZO

Jedwali 1: Mifugo katika Nyakatoke............... 9

Jedwali 2: Viwango vya Elimu Nyakatoke...... 12

Jedwali 3: Huduma za Matibabu..................... 14

Jedwali 4: Uzalishaji Binafsi............................ 16

Jedwali 5: Wakazi wa Nyakatoke.................... 24

Jedwali 6: Koo za Nyakatoke........................... 25

# UTANGULIZI

Ripoti hii ni sehemu ya utafiti kuhusu Bima za Kijamii, Umaskini na Marekebisho ya Uchumi uliofanyika katika kitongoji cha Nyakatoke mkoani Kagera, kati ya Desemba 1999 na Desemba 2000. Bima za Kijamii zisizo rasmi hujitokeza katika jamii kama mbinu za kupambana na matatizo na kukidhi haja mahsusi. Aina na muundo wa mifumo hii hutofautiana kati ya jamii na nyingine kulingana na hali halisi ya jumuiya kijiografia, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia. Kwa hiyo utafiti wa mifumo ya bima zisizo rasmi, sharti uzingatie vigezo hivi katika jamii husika.

Lengo la ripoti hii ni kutoa picha ya jumla ya Nyakatoke kijamii na kiuchumi ambayo ilikuwa kichocheo cha kuwepo mifumo mbali mbali na mshawasha wa kubuni na kuiga mifumo hiyo. Uchambuzi wa miundo mahsusi ya bima za kijamii zisizo rasmi ndani ya Nyakatoke, mahusiano yake na umaskini pamoja na mabadiliko ya kiuchumi katika miaka kumi iliyopita, umo katika ripoti zitakazofuata za Bw. Joachim De Weerdt na Bi. Katleen Van Den Broeck.

Kwa kutambua kwamba utafiti hautakuwa na maana kama matokeo yake hayatawafikia wanajumuiya husika, imeonekana ni vema kujumuisha katika ripoti hii ya Kiswahili* baadhi ya taarifa na takwimu kutoka utafiti wa dodoso, ambazo kiutaratibu zilipaswa kutolewa katika ripoti ya mwisho. Kwa kuwa ripoti hiyo itakuwa ya Kiingereza na ya kitaalamu zaidi, imeonekana ni vema pia kutoa maelezo ya ziada kwa majedwali na vielelezo katika ripoti hii ya Kiswahili. Nia ni kuwafikishia ujumbe huu wengi wa

---

* Ripoti hii iliandaliwa awali kwa lugha ya Kiingereza na kutafsiriwa pamoja na kuongezewa vipengele vilivyoonekana kuwa muhimu kwa walengwa wa ripoti hii.

wakazi wa vijijini, hususan wananchi wa Nyakatoke na maeneo ya Rubale kwa jumla.

Ripoti hii kimsingi ni matokeo ya mahojiano yasiyo rasmi yaliyofanyika Nyakatoke na vitongoji jirani mnamo Desemba 1999, yaliyoiwezesha timu yetu (waandishi pamoja na Joachim De Weerdt) kupata taarifa za awali kuhusu jumuiya hii. Viongozi, wazee na watu wengine wanaoijua Nyakatoke walitoa mchango wao bila kusita. Baada ya kurudi Bukoba, ilifanyika kazi ya kusoma nyaraka na vitabu husika. Mwezi Aprili 2000, mmoja wetu alirudi kwa nia ya kukusanya taarifa kuhusu historia ya Nyakatoke. Kama mwanzo, wazee na wanaoijua Nyakatoke (wa ndani na nje ya kitongoji) walihojiwa; majibu na maoni yao kwa pamoja ndiyo msingi wa sura inayozungumzia historia.

Kila mada katika ripoti hii imetazamwa kwa kuzingatia mchango na athari zake kwa kilimo. Hii ni kwa kutambua kuwa Nyakatoke, kama jumuiya nyingine za vijijini, inategemea sana kilimo.

Sehemu kulikofanyika utafiti inajumuisha kitongoji cha Nyakatoke na familia chache kutoka kitongoji jirani cha Nyakalaaro, ambazo zimeonekana kuwa na ushirikiano wa karibu zaidi na Nyakatoke. Hivyo kwa matumizi ya utafiti huu maneno **Nyakatoke** na **kitongoji** yanamaanisha jamii hii kwa pamoja, na si sawa na yanavyotumika kiutawala.

# 1. JIOGRAFIA, UDONGO NA MVUA

## 1.1. Mahali ilipo

Mkoa wa Kagera ambamo Nyakatoke inakutwa, upo kaskazini –magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Upo kati ya latitudo 1° 00' na 2° 45' kusini mwa Ikweta, na kati ya 30° 25' na 31° 48' mashariki ya mstari wa Greenwich. Kwa upande wa kaskazini unapakana na nchi ya Uganda, magharibi kuna nchi za Rwanda na Burundi, na mashariki ni Ziwa Victoria. Kusini unapakana na mikoa ya Kigoma na Shinyanga.

Nyakatoke ni kitongoji katika kijiji cha Rubale, kata ya Rubale, tarafa ya Rubale katika wilaya ya Bukoba vijijini Mkoani Kagera. Rubale ipo umbali wa kilometa 60 toka Bukoba mjini. Nyakatoke iko umbali wa kilometa 15 hivi kusini mwa Ziwa Ikimba, kando ya barabara itokayo Rubale kuelekea maeneo ya Burigi, kiasi cha kilometa 3 kusini ya makao makuu ya Kata na Tarafa Rubale. Kitongoji hiki kina eneo la kilometa za mraba 1.6.

Nyakatoke ipo kwenye eneo linalojulikana kama Nyanda za Chini za Bukoba na Muleba, kwenye ukingo wa mashariki wa bonde la Burigi-Ikimba. Ipo kwenye mwanzo wa mwinuko kuelekea kwenye uwanda wa juu wa Kamachumu kwenye Nyanda za Juu za Muleba. Kijito kitokacho

milimani upande wa mashariki hukatiza kitongoji hiki kuelekea kwenye tingatinga upande wa magharibi. Mbuga inatenganisha Nyakatoke na kitongoji cha Nyakaju upande wa kaskazini, na kwa upande wa kusini mashamba yaliyotawanyika ya wahamiaji wapya yanakitenganisha na kitongoji cha Nyakalaaro. Vilimani upande wa mashariki kuna Kashasha na Mbugwe, ambavyo ni vitongoji vya vijiji jirani.

## 1.2. Udongo na Mvua

Nyanda za chini za Bukoba na Muleba ni eneo lenye rutuba ya wastani, lakini iliyo bora kuliko ya ardhi zilizochoka za kaskazini na mashariki, jambo linalosababisha wahamiaji kuja katika eneo hili.

Kama ilivyo katika maeneno mengine ya mkoa wa Kagera, kuna vipindi vinne vya majira ya mwaka, viwili vya mvua na viwili vya jua. Januari na Februari ni *Kanda*[1] au kipindi kifupi cha jua, kinachofuatwa na kipindi kifupi cha mvua nyingi za masika au *Toigo*[2] kati ya mwezi Machi na Mei.  Kuanzia mwezi Juni hadi Septemba ni kipindi kirefu cha kiangazi au *Kyanda*[3], kikifuatiwa na kipindi kirefu cha vuli au

---

[1] ***Kanda*** ni kipindi kifupi cha jua kati ya Januari na Februari.  Kipindi hiki huwawezesha wakulima kukausha mazao ya msimu wa vuli, hasa maharage.

[2] ***Toigo*** ni kipindi cha mvua nyingi kati ya mwezi Machi na Mei. Kipindi hiki baadhi ya wakulima hupanda mazao yao ya msimu. Mara kwa mara barabara nazo hupitika kwa shida.

[3] ***Kyanda*** ni kipindi cha jua kali kuanzia mwezi Juni hadi Septemba.  Tofauti na kiangazi cha sehemu nyingine za nchi, katika mwaka wa kawaida hunyesha mvua angalao mara moja katika kila wiki tatu hadi nne muda wote wa kipindi hiki

M*uhanguko*[4], chenye mvua za wastani, kuanzia Septemba hadi katikati ya Januari. Kuna vipindi viwili vya kupanda, lakini mazao mengi hupandwa wakati wa vuli kuliko wakati wa masika.

Eneo hili halina mvua nyingi likilinganishwa na maeneo ya kaskazini na yale ya mwambao wa ziwa.(taz. Ambatisho C). Hali ya mvua imekuwa si ya kuaminika kwenye miaka ya karibuni. Tangu mvua za *El-Nino* [5]za mwaka 1997, hali imebadilika. Mvua hazinyeshi kwa wakati, na zinaponyesha haziwi za kutosha. Uzalishaji wa ndizi, ambacho ndicho chakula kikuu, umeathirika sana, na hali ya chakula inazidi kuwa ya wasiwasi kutokana na kuibuka ugonjwa ushambuliao mihogo (CMD-ugv)[6] ambacho ni chakula cha pili cha kutegemewa.

## 2. UMILIKAJI NA UTUMIAJI WA ARDHI

### 2.1. Sheria za Umilikaji

[4] ***Muhanguko*** ni kipindi cha mvua kati ya Septemba na Januari; ndicho kipindi kinachopendelewa kwa kilimo cha mazao ya muda, hususan mahindi na maharage.

[5] ***El-Nino*** ni machafuko ya hali ya hewa yanayoambatana namvua nyingi kupita kiasi na mafuriko makubwa.

[6] **CMD-ugv** ( Cassava Mosaic Decay- Uganda Variant) ni ugonjwa wa mihogo unaoshambulia majani yake na kuifanya isitoe mazao mazuri.

Kisheria, ardhi nchini Tanzania humilikiwa na Taifa kwa matumizi ya wananchi wanapoihitaji. Mtu huwa na haki juu ya ardhi anayoitumia. Enzi za Ujamaa, ardhi ilichukuliwa kuwa si mali ambayo ingeweza kuuzwa na kununuliwa. Mashamba hakika yaliweza kurithiwa, kuuzwa au kununuliwa, lakini kila mara ilisisisitizwa kwamba kilichouzwa yalikuwa ni mazao na wala si ardhi yalimopandwa.

Sambamba na sheria za taifa kuhusu ardhi, umilikaji wa ardhi, hasa maeneo ya vijijini, uliendelea kwa kiasi fulani kutawaliwa na sheria za kijadi. Tofauti na sera za kitaifa kuhusu ardhi, Wahaya muda wote waliamini ardhi kuwa kipimo cha hadhi ya mmilikaji, chimbuko la usalama wa mtu na kitambulisho chake. Ardhi daima imekuwa ikiuzwa na kununuliwa. Kila ukoo ulikuwa na ardhi yake ambayo ilirithishwa kwa watoto wa kiume. Wasichana waliweza kurithi mashamba ya baba zao, lakini kwa kipindi cha uhai wao tu. Baada ya kufariki ardhi ilirudi mikononi mwa ukoo; wasingeweza kuwarithisha watoto wao, kwani hawa ni watu wa ukoo mwingine (ukoo wa baba zao)

Buhayani ardhi isingeweza kuuzwa bila kibali cha ukoo. Hata pale zilipokuwapo sababu za kutosha ardhi kuuzwa, wanaukoo walipewa kipaumbele kuinunua kwa minajiri ya kuhakikisha haiendi nje ya ukoo, na iliweza kununuliwa na mtu wa nje pale tu ambapo ukoo

uliridhika kwamba hakuna mtu miongoni mwao wa kuinunua.

Katika Nyakatoke ya leo, mfumo wa umilikaji ardhi umelegezwa. Kama kwingineko Buhayani, sheria za kitaifa kuhusu ardhi hazikuweka mizizi hasa, kwa vile kilimo cha mazao ya kudumu kama vile migomba na kahawa kilimhakikishia mtu kudumu na ardhi aliyoilima. Ardhi iliyokuwa imebaki huru kugawiwa na serikali mara nyingi ilikuwa haina rutuba, na kwa sasa karibu yote ina wamiliki, kasosro milimani na kwenye tingatinga.

Mamlaka ya kijadi ya koo kusimamia umilikaji na uuzaji wa ardhi yamemomonyoka haraka mbele ya uchumi wa kifedha. Ardhi iliyo nyingi katika maeneo haya imenunuliwa na wahamiaji kutoka kwa wakazi wa awali. Wauzaji wasingeweza kubanwa na Sheria za jadi kwa vile ukoo una mamlaka juu ya ardhi kama ilipatikana kwa kurithiwa tu. Kwa sasa Nyakatoke watu wanaweza kubadilishana ardhi kibiashara, hasa katika maeneo yaliyokaliwa hivi karibuni, ambapo wamiliki bado wana madaraka kamili juu ya ardhi yao kwa vile ni wamiliki wa awali. Hata wachungaji ambao waliishi kwenye ardhi waliyogawiwa bure na kijiji kwa miongo miwili tu, waliweza kuuza ardhi yao wakati wa kuondoka! Kwa ujumla nguvu za ukoo juu ya ardhi zimepungua sana.

Hata sheria za urithi zinabadilika haraka. Kwa sasa kuna wanawake saba waliokalia mashamba waliyorithi kwa baba zao au waume zao. Kwa hali ilivyo sasa, haitakuwa rahisi kwa ukoo kuwafukuza watoto wao, hasa ikizingatiwa sheria mpya ya urithi inayowapa haki sawa wasichana na wavulana katika maswala ya urithi (ikiwemo na ardhi), ikiwa ni pamoja na haki ya kurithisha watoto wao mali ambayo walirithi.

Karibu kila kaya katika Nyakatoke inamiliki ardhi inayoikalia na kuilima. Kuna familia chache za kupita, kama vile vibarua na wajane wazee wasio na ndugu, wanaoishi katika mashamba wasiyoyamiliki. Kulingana na makubaliano na wenye mashamba, watu kama hawa huweza kufanya baadhi ya shughuli katika mashamba hayo na kupewa haki ya baadhi ya mazao.

## 2.3. Matumizi ya Ardhi.

Matumizi ya ardhi yanaweza kugawanywa katika aina tatu. Kwanza ni *kibanja*[7], ambalo ni eneo linaloizunguka nyumba lililopandwa mazao ya kudumu, hasa migomba na mibuni. Haya ni

---

[7] ***Kibanja*** (uw.*bibanja*) shamba ambalo kwamo ukutwa mazao ya kudumu, hasa migomba na mibuni. Aghalabu hupandwa pia mazao mengine hususan mahindi na maharage wakati wa msimu. Kibanja huwa katika sehemu yenye rutuba nzuri ya ardhi ya kaya.

matumizi muhimu sana, na mara nyingi *kibanja* huwa katika eneo lenye rutuba ya kutosha. Kibanja ni kipimo cha hadhi ya mmiliki, kinachompa heshima na kumpa hadhi ya ukazi wa kudumu. *Kibanja* pia humpa mtu usalama, kwani mazao yake ya kudumu yanaweza kuzalishwa kwa huduma na nguvu pungufu yakilinganishwa na mazao ya msimu.

Kuzunguka *kibanja* linaweza kuwapo eneo la *kikamba* [8]ambalo huweza kutumika kwa mazao ya msimu, kama vile mihogo, viazi, karanga, mahindi na maharage. Kikamba mara nyingi huwa na rutuba ya wastani, na kadri familia zinavyoongezeka, taratibu hupandwa migomba na mibuni na kubadilika kuwa *kibanja*. Kwa sehemu kubwa, hili limekwisha fanyika Nyakatoke; sehemu ndogo za kikamba zilizobaki ni kwenye maeneo ya wahamiaji wapya, au zile zinazoonekana kupungukiwa rutuba kiasi cha kutoweza kuotesha vizuri migomba na mibuni.

Tatu kuna *rweya*[9], ambayo ni mbuga wazi ilizozunguka makazi. Kawaida hutumika kwa

---

[8] ***Kikamba*** (uw. *bikamba*) Sehemu iliyo karibu na kibanja ambayo haina mazao ya kudumu. Hutumika kwa kilimo cha mazao ya muda au kupumzishwa. Sehemu hii huwa na rutuba ya wastani.

[9] ***Rweya*** (uw.*nyeya*) Nyika zenye rutuba kidogo ambazo kiutamaduni hutumika kwa malisho ya mifugo na kilimo cha mazao yasiyohitaji rutuba nyingi. Miaka mingi ya kupunguzwa virutubisho kwa kulishwa mifugo, ukataji

malisho na kilimo cha mazao ya msimu, hasa yasiyohitaji rutuba nyingi kama vile mihogo na njugu mawe.  Baadhi ya ardhi bado iko mikononi mwa serikali, na inaweza kugawiwa kwa wahitaji.  Hata hivyo ni wachache wanaoona umuhimu wa kumiliki ardhi kwa ajili ya mazao ya muda, hali kila mmoja ana haki ya kupata pa kulima anapohitaji.  Baadhi ya familia zina mashamba ya miti kwenye maeneo ya *rweya* yaliyo karibu na mashamba yao.

Karibu ardhi yote nzuri katika Nyakatoke inamilikiwa na mtu.  Ardhi iliyobakia kuwa ya jumuiya haina rutuba (milimani na kwenye tingatinga). Kadri idadi ya watu inavyoongezeka, historia inaweza kujirudia: Familia mpya zitalazimika kuhamia kwingineko kutafuta ardhi yenye rutuba.

Hakuna ushahidi wowote wa kukodisha ardhi kwa malipo.  Upeanaji wa ardhi (*kikamba* na *rweya)* kwa ajili ya mazao ya muda ni jambo la kawaida kati ya marafiki na majirani.  Kiasi kidogo cha mavuno kinaweza kutolewa kwa mwenye ardhi kama shukrani kwa matumizi ya ardhi yake.

## 3. KILIMO NA UFUGAJI

---

nyasi kwa ajili ya kuezekea, kutengenezea pombe na kutandaza majumbani na mashambani na uchomaji moto ovyo kumezifanya sehemu hizi kuhitaji mbolea nyingi kwa kilimo cha mazao ya kudumu.

## 3.1. Kilimo.

Nyakatoke, kama maeneo mengine ya Buhaya, maisha yake yanategemea sana kilimo cha migomba na mibuni katika *kibanja.* Kilimo mchanganyiko kimefanyika kwa kiasi fulani katika kibanja kwa kuongeza mazao kama magimbi, viazi vikuu na mihogo, hasa sehemu za pembezoni mwa shamba au katika mashamba yasiyostawisha vema migomba. Mazao yaliyo mengi ya mihogo na viazi hulimwa tofauti kwenye *kikamba* na *rweya*. Mahindi na maharage daima hupandwa kwenye migomba mbali na yalimwayo kwenye *kikamba* na *rweya.*

Ardhi ina rutuba ya kutosha, na athari za *kihuka* [10](weevil) na *panama* [11]hazijasambaa sana ukilinganisha na maeneo ya ziwa penye unyevu zaidi. Uzalishaji wa ndizi, hasa katika miaka ya karibuni, umeathiriwa na ukosefu wa mvua ya kuaminika. Hata katika mwaka wa kawaida, uzalishaji wa ndizi katika maeneo haya hupanda na kushuka kulingana na majira, kunakosababishwa na mvua pungufu ya wastani

---

[10] ***Kihuka*** (uw. *bihuka*) Mdudu anayetaga mayai yake kwenye shina la mgomba(banana weevil).Viwavi wake hutoboa toboa shina na kuufanya mgomba udhoofike na hata kufa kabisa.

[11] ***Panama*** – Ugonjwa wa migomba unaosababishwa na virusi. Huufanya mgomba kudhoofika, majani yake kugeuka njano na mwisho kufa kabisa.

na kiangazi kirefu. Hupatikana ndizi nyingi kati ya Mei na Septemba, na kushuka ghafla kati ya Oktoba na Aprili.

Upungufu huu wa chakula muhimu hudhibitiwa kwa kutumia mazao ya muda, hasa mihogo, maharage na viazi vitamu. Madhara ya upungufu huu yanaweza kuwa mabaya zaidi siku za usoni kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa mihogo (CMD - ugv) ambao umefuta matumaini ya mavuno tosha ya mihogo mwaka huu. Kampeni ya kupanda mazao mengine kama viazi vikuu, magimbi na viazi mviringo kupunguza makali ya kuharibika kwa mihogo bado haijapokelewa ipasavyo.

Nyakatoke na maeneo ya jirani huzalisha kwa wingi mazao mengi ya msimu, hasa maharage, mahindi, karanga, njugu mawe na mazao ya mboga kama nyanya, *ntongo*, na kabechi. Udongo wake usioosheka hufaa sana kwa kilimo cha mazao haya kiasi cha kuyafanya mazao ya biashara baada ya kahawa, ambayo mbali na kustawi vema, haioteshwi kwa wingi kama maeneo mengine ya Bukoba, Muleba na Karagwe. Sababu zinazotolewa na wengi ni kuwa wahamiaji hutoa kipaumbele kwa mazao ya chakula.

Maharage na mahindi hayakustawi vizuri kipindi cha 1999-2000, sababu zinazotolewa na wengi ni upungufu wa mvua. Sehemu za kusini mwa

kitongoji na sehemu ya kaskazini mwa mto zimepata mavuno ya wastani, wakati zile za katikati zimeambulia mavuno hafifu. Mavuno ya karanga pia hayakuwa mazuri shauri ya hali ya hewa, yakiwa yamefanywa mabaya zaidi na wanyama waharibifu.

**3.2. Mifugo.**

Nyakatoke ina kiasi kizuri cha mifugo, mikubwa kwa midogo. Aprili mwaka 2000 kulikuwa na jumla ya ng'ombe majike wa kienyeji 51 katika familia 10 na wa maziwa watano katika familia tatu. Pia kulikuwa na madume watano katika familia tatu na ndama 20 katika familia 10. Wafugaji bado hawajabuni mfumo mzuri wa kuogesha mifugo tangu kukoma kwa utaratibu wa ruzuku ya serikali ya dawa za kuogesha mifugo.

Kila mfugaji huosha mifugo yake nyumbani wakati josho halina kazi. Utaratibu huu si toshelevu, kwani uthibiti wa kupe waweza kuwa mgumu kama baadhi ya wafugaji katika kundi watashindwa kuogesha mifugo yao ipasavyo. Kulikuwa na kuku na bata wengi, wakifikia jumla ya 352 katika familia 73, jumla ya mbuzi na kondoo katika kitongoji ni 197 katika familia 60 na nguruwe 11 katika familia tatu. Aidha kulikuwa na sungura na njiwa wachache

**JEDWALI 1: Mifugo katika Nyakatoke**

| Aina | Idadi ya mifugo | | Idadi ya familia zinazoimiliki | Idadi ya familia zinazoitunza |
|---|---|---|---|---|
| | Inayotunzwa na mmiliki | Inayotunzwa na asiye mmiliki | | |
| Madume** | 2 | 3 | 2 (1.4%) | 3 (1.8) |
| Ng'ombe wa maziwa* | 2 | 3 | 2 (1.4%) | 3 (1.8) |
| Ng'ombe wa kienyeji* | 18 | 33 | 7 (5.0%) | 10 (6.1) |
| Ndama** | 11 | 9 | 7 (5.0%) | 10 (6.1) |
| Mbuzi | 137 | 58 | 48 (34.3%) | 58 (35.4) |
| Kondoo | 1 | 1 | 1 (0.7%) | 2 (1.2) |
| Nguruwe | 3 | 8 | 2 (1.4%) | 3 (1.8) |
| Kuku | 290 | 14 | 57 (40.7) | 59 (36.0) |
| Bata | 41 | 7 | 12 (8.6%) | 14 (8.5) |

Takwimu hizi zimekusanywa na utafiti huu Februari 2000

* Majike

** Inajumuisha wa kienyeji na kisasa

# 4. MIUNDO-MBINU, MASOKO NA BIASHARA

## 4.1. Mawasiliano.

Tofauti na jamii zilizopo karibu na miji au karibu na barabara kuu, jamii nyingi za vijijini zina uhaba wa miundombinu. Barabara (hasa kwenye majira ya mvua) ziwaunganishazo na makao makuu ya mikoa na wilaya huwa mbovu. Hii huwatenganisha na masoko haya pamoja na makubwa zaidi ya nje. Kwa kiasi kikubwa hii huwaathiri katika kupata bidhaa na huduma nyinginezo zilizoko mbali nao, na kuwapunguzia uwezekano wa kuuza mazao yao.

Nyakatoke imeunganishwa na mji wa Bukoba, ambao ni makao makuu ya mkoa na wilaya kwa barabara ya changarawe inayoachana na barabara kuu ya Bukoba-Biharamulo sehemu ya Kyetema karibu na bandari ya Kemondo. Barabara hii huchafuka na kupitika kwa shida sana nyakati za mvua. Kuna barabara zinazounganisha Nyakatoke na miji midogo ya Kyaka na Mutukula mpakani mwa Uganda kupitia pande zote za Ziwa Ikimba. Barabara ndogo itokayo Rubale kuelekea maeneo ya Burigi hupitia kijijini hapa. Barabara itokayo Rubale hupanda mlimani Kamachumu ambapo tawi moja huelekea kaskazini hadi Bukoba, na jingine kusini kupitia Nshamba hadi Muleba kwenye barabara kuu ya

Bukoba–Biharamulo. Huduma za posta na simu hupatikana Kamachumu.

## 4.2. Elimu.

Kijiji cha Rubale kina shule tatu za karibu zinazokihudumia. Mbili za msingi na shule moja ya sekondari ya Serikali, zote zikiwa umbali wa kilometa kama mbili hivi kaskazini mwa Nyakatoke, kwenye barabara ielekeayo Rubale kituoni. Pia Shule ya Msingi Rukoma katika kijiji Rukoma hutumiwa na baadhi ya wakazi wa Nyakatoke.

Inaaminika kuwa katika jamii za Kihaya, walio wengi walijaliwa kufuta ujinga mapema hata kabla hatujapata uhuru. Mafanikio haya yalikuwa kwa kiasi kikubwa matokeo ya kuingia wamisionari katika Bukoba mwishoni mwa karne ya 19 na kufungua shule nyingi, zikiwemo za msingi, sekondari pamoja na vyuo. Baada ya uhuru, kampeni za Elimu ya Watu Wazima zilisaidia kuondoa ujinga miongoni mwa wale ambao hawakupata bahati ya kwenda shule. Hata hivyo hali ya kujua kusoma na kuandika inaonekana kufifia mwishoni mwa karne ya 20 kama ilivyo sehemu nyingi hapa nchini, japokuwa maeneo yaliyokuwa nyuma yanajinyanyua kwa kasi.

Utafiti uliofanywa na timu yetu Nyakatoke kwa njia ya dodoso mnamo Februari 2000 ulizingatia

viwango vya elimu ya wakazi wote wa kitongoji wenye umri kuanzia miaka 15 na kuendelea. Kati ya jumla ya watu 298 waliohojiwa, ni 48.7% waliohitimu elimu ya msingi. Kati yao 23.2% ama bado wanasoma au hawakumalizia elimu ya msingi. Kiasi cha 9.1% wamepata elimu ya sekondari, ambapo kati yao 8.1% ni kati ya kidato cha kwanza na cha nne, na 1% wamefikia kidato cha sita. Hakupatikana mtu hata mmoja ambaya ni mkazi wa kudumu wa Nyakatoke aliyehojiwa ambaye amefikia elimu ya chuo kikuu. Hata hivyo kuna 1.3% waliopata mafunzo ya ujuzi/ufundi wa aina mbali mbali. Cha kushangaza ni kuwa watu wazima waliopitia Elimu ya Watu Wazima ni 2.7% ya waliohojiwa, wakati takwimu zinaonyesha wasojua kusoma wala kuandika ni karibu mara sita zaidi, yaani 15.1% ya waliohojiwa.

Ikizingatiwa kwamba Mkoa wa Kagera ulikuwa kati ya mikoa iliyokuwa na mafanikio makubwa katika kampeni za kufuta ujinga nchini, kiwango cha wanaojua kusoma na kuandika Nyakatoke cha 84.9% tu hakilingani na mategemeo.

**JEDWALI 2: Viwango vya Elimu Nyakatoke**
(Umri miaka 15 na kuenelea)

| KIKUNDI | IDADI | ASILIMIA YA KUNDI |
|---|---|---|
| Wasiojua kusoma wala kuandika | 45 | 15.1% |
| Wasiomalizia Elimu ya Msingi (bado wanasoma au wamemaliza shule) | 69 | 23.2% |
| Waliohitimu Elimu ya Msingi | 145 | 48.7% |
| Kidato cha kwanza hadi cha nne | 24 | 8.1% |
| Waliofikia Kidato cha sita | 3 | 1.0% |
| Elimu ya Watu Wazima | 8 | 2.7 |
| Mafunzo mengineyo | 4 | 1.3% |
| Elimu ya Chuo Kikuu | 0 | 0.0% |
| JUMLA waliohojiwa (Umri miaka 15 na kuendelea) | 298 | 100% |
| JUMLA wasiohojiwa (Umri chini ya miaka 15) | 303 | - |
| JUMLA Wakazi wote | 601 | - |

Takwimu hizi zimekusanywa na wenyewe Februari 2000

## 4.3. Afya

Afya ya jamii hutegemea mambo mengi, yakiwemo lishe, hali ya hewa, usafi wa mwili na mazingira pamoja na matibabu. Jamii nyingi hasa za vijijini, hukumbwa na upungufu au ukosefu wa huduma za afya. Kasoro hizo husababishwa na uhaba wa vituo vya kutoa huduma hizo, yaani zahanati, vituo vya afya na hospitali.Gharama za kulipia matibabu pia huwa kikwazo kikubwa kwa familia za kawaida. Aidha umbali wa kufika sehemu zinapopatikana huduma hizo huchangia katika kuwakosesha wananchi misaada ya matibabu.

Kitongoji kina vyanzo vitatu muhimu vya maji. Viwili ni chemichemi kwa upande wa magharibi, cha tatu ni kijito (Kalesilwengonzi) kinachotokea milimani na kukatisha kijijini kuelekea magharibi. Mfumo wa *gravity* [12]hukinga maji haya na kuyasambaza kwenye kijiji cha Rubale. Kuna mabomba mawili ya jumla kitongojini Nyakatoke.

Kwa huduma za afya, kuna zahanati ya Rubale na kituo cha afya Izimbya, takribani kilometa 12

---

[12] ***Gravity*** - Mfumo wa ugavi wa maji ya bomba ambapo maji huchukuliwa kwenye chanzo kilicho kwenye mwinuko na kusukumwa kwa nguvu za uzito wake hadi kwa watumiaji bila ya kutumia mashine.

magharibi. Kuna hospitali za misheni za Ndolage (Walutheri) na Rubya (Wakatoliki), zote mbili zikiwa umbali wa kilometa 35 hivi kutoka Rubale. Hospitali ya Mkoa iko umbali wa kilometa 60 mjini Bukoba.

Katika jamii ya Nyakatoke yameripotiwa matukio 97 ya kuugua kuanzia Desemba 1999 hadi Juni 2000. Taarifa kuhusu wagonjwa hao zimeonyeshwa katika Jedwali 3. Kati ya wagonjwa hao 37.1% walitibiwa kwa madawa toka madukani au magulioni. Kiasi cha 26.8% waliitumia vema zahanati ya serikali ya Rubale, wakati kituo cha afya Izimbya na hospitali ya Ndolage ziliendewa kila moja na 5% ya waliougua. Vituo vya afya vilivyo mbali na jamii hii, ikiwa ni pamoja na hospitali ya mkoa Bukoba, hospitali ya Rubya na vingine kwa pamoja vilihudumia kadri ya wagonjwa sawa na 3% kati yao. Kati ya wagonjwa wote 12.4% walitibiwa kwa dawa za kienyeji.

**JEDWALI 3: Huduma za Matibabu**

| WALIPOTIBIWA | IDADI YA WAGONJWA | ASILIMIA YA WAGONJWA |
|---|---|---|
| Wasiopata huduma | 8 | 8.2 |
| Dawa za kienyeji | 12 | 12.4 |
| Maduka ya Madawa | 36 | 37.1 |
| Zahanati Rubale | 26 | 26.8 |
| Kituo cha Afya Izimbya | 5 | 5.2 |
| Hospitali Ndolage | 5 | 5.2 |
| Hospitali Rubya | 1 | 1.0 |
| Hospitali ya Mkoa | 1 | 1.0 |
| Vituo vingine | 1 | 1.0 |

| | | |
|---|---|---|
| Haijulikani walipotibiwa | 2 | 2.1 |
| JUMLA | 97 | 100 |

Takwimu hizi zimekusanywa na wenyewe Februari 2000

Katika mahojiano zaidi na wale ambao hawakupata huduma ya nje, sababu iliyotajwa na wengi (50%) ilikuwa ni gharama kubwa ya matibabu. Hii inaashiria kuwa hawakuweza kutafuta huduma hiyo kwa sababu ya kutomudu gharama zinazotakiwa. Imeshindikana kueleweka ni kwa nini watu hawa hawakwenda zahanati ambako huduma hutolewa bure. Baadhi waliongelea swala la kuchoshwa na magonjwa yao na hivyo kukata tamaa ya kutibiwa hospitalini. Wengine walionyesha imani ya kuwa haikuwa lazima kwenda hospitali, hasa kwa magonjwa madogo madogo.

## 4.4. Masoko na Biashara

Baadhi ya familia zinatoa huduma ya kuuza bidhaa muhimu kwa matumizi ya nyumbani, kama vile chumvi, sabuni, mafuta ya taa, sigara, n.k. Maduka makubwa zaidi yanapatikana kwenye kituo cha Rubale.

Wanajumuiya huuza mazao yao mengi kama vile nafaka, mboga, matunda na pombe magulioni. Magulio muhimu ni Rukoma (Alhamisi, km 5), Rubale (Jumamosi, km 3) Izimbya (Jumanne, km 12) na Kilamba (Jumapili, km 15). Pia wafanyabiashara wadogo wadogo wa bidhaa zisizo za kilimo kama nguo za mitumba na bidhaa ndogondogo za matumizi ya nyumbani hutumia magulio kupanua soko lao. Wakulima wa mazao ya mboga, hasa nyanya na *ntongo* [13]nao hutembeza kwenye magulio haya, na wakati mwingine hata kwenye masoko ya mbali ya Kamachumu na Nshamba.

Kahawa huuzwa kupitia kwenye kituo cha chama cha msingi cha ushirika kilichopo Migara. Yapo pia mashirika binafsi ambayo hununua kahawa kwa kuweka vituo vya muda Rubale na vijiji

---

[13] ***Ntongo***- Mboga aina ya matunda meupe na chungu kidogo, inayopendwa sana mkoani Kagera. Wengine huita nyanya mshumaa.

jirani. Pia wanunuzi wadogo wadogo, *bayeki*[14], huzunguka nyumba hadi nyumba wakinunua mahindi na maharage wakati wa msimu.

---

[14] ***Bayeki*** (um. *muyeki*)- Ni neno ambalo katika maeneo ya Rubale humaanisha vijana ambao mara kwa mara hawatumii mitaji yao binafsi wanaowafanyia matajiri biashara za kuuza na kununua hasa hasa mazao. Ujira wao hutokana na kubadili bei na vipimo walivyokubaliana na tajiri wao.

## 4.5. Nguvukazi

Maendeleo ya jamii yoyote ile yanategemea uzalishaji mali wake pamoja na uwiano kati ya uzalishaji na utumiaji. Hata katika familia, maendeleo yanaweza kuwa ya kasi au kuzorota kutegemea ni watu wangapi katika familia hiyo wanazalisha na kutumia, na ni wangapi wanatumia bila ya kuzalisha. Mlinganyo huu unaweza kutoa picha juu ya maendeleo, kwani pale ambapo wazalishaji ni wachache mno wakilinganishwa na walaji, si rahisi kupata ziada ambayo huhitajika katika kusukuma mbele maendeleo.

Katika utafiti wa dodoso uliofanyika Nyakatoke, ambao matokeo yake yanaonyeshwa katika JEDWALI 4, watu 291 walio na umri kuanzia miaka 15 na kuendelea walihojiwa kuhusu uzalishaji mali. Kati yao ni 84.2% wenye pato binafsi. Hii ni sawa na 40.8% ya wakazi wote wa kitongoji. Kwa ufupi ni kwamba watu 245 ndiyo wanaotegemewa kutosheleza mahitaji ya jamii nzima yenye jumla ya watu 600.

**JEDWALI 4: Uzalishaji Binafsi**

| KUNDI | IDADI | Asilimia ya Waliohojiwa | Asilimia ya Jamii nzima |
|---|---|---|---|
| Wenye pato binafsi | 245 | 84.2 | 40.8 |
| Wasio na pato binafsi | 46 | 15.8 | 7.7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JUMLA waliohojiwa (Umri miaka 15 na kuendelea) | 291 | 100 | 48.5 |
| Wasiohojiwa (Umri chini ya miaka 15) | 310 | - | 51.5 |
| JUMLA wakazi wote | 601 | - | 100 |

Takwimu hizi zimekusanywa na wenyewe Februari 2000

# 5. HISTORIA FUPI YA NYAKATOKE:

## 5.1. Makazi ya awali

Tofauti na nyanda za Juu za Bukoba na Muleba pamoja na maeneo ya ukanda wa ziwa, nyanda za chini zimekaliwa hivi karibuni. Baadhi ya wakazi wa maeneo haya ambao wangali hai hadi hivi leo wanathibitisha kwamba wahamiaji wa mwanzoni mwa karne ya 20 walibugudhiwa sana na wanyama wakali, hasa simba. Wakazi wa Nyakatoke, Kashasha na Kikomero walilazimika kwenda Kabirizi (wakati ule ikiwa *Gombolora*[15]) wakiwa na silaha na katika makundi kwa ajili ya usalama.

Kwa karne nyingi, sehemu za kaskazini mwa Kagera, yaani Bukoba, Muleba na Karagwe zikikaliwa na wahamiaji kutoka kaskazini, walioingia kwa kuvuka mto Kagera au kwa mitumbwi kupitia Ziwa Victoria. Kwa hiyo sehemu za kwanza kukaliwa na watu wengi zilikuwa ni Kiziba (kaskazini) na Bugabo (kaskazini mashariki) zilizo katika wilaya ya Bukoba Vijijini, pamoja na mwambao wa ziwa na nyanda za juu za Bukoba na Muleba.

Bado haijulikani kwa uhakika ni lini mtu wa kwanza aliishi Nyakatoke, lakini kuna ushahidi

---

[15] ***Gombolora***-Eneo la utawala wakati wa mkoloni mkoani Kagera. Ukubwa wake ungelingana na Kata.

unaoonyesha kuwa eneo hili lilianza kukaliwa mwanzoni mwa karne ya ishirini.

Kwanza, kulingana na kauli ya wazee kadhaa wa Nyakatoke, kuna familia nne zilizokuwapo Nyakatoke kwenye mwaka wa 1910. Familia hizi ni ya Matundwe (Muhunga) iliyoishi kwenye shamba ambalo hivi sasa linakaliwa na Mzee Francis Myaka na nduguye Mwalimu Benjamini Mutembei. Familia ya pili ni ya Kahyo babake Kibogoyo (Musimba) ambaye kizazi chake hakipo tena, na ambaye aliishi kwenye shamba linalomilikiwa na Mwalimu Lucas Rwabishugi lililo nyuma ya Ma Roosa Kamakumbi. Familia ya tatu ni ya Rwenduuru (Muhunga) baba yake Ma Laurencia na Marehemu Ma Miriana ambaye shamba lake liko kati ya mashamba ya Mzee Leopold Munyambo na Yakobo Matoju. Familia ya nne ni ya Mushaki Kankeera Kaboro k'Eihwa, ambaye baadaye alihamia maeneo ya Butakya, lakini wakati ule aliishi kwenye shamba anamokaa Adam Abdulatif na Kassim Selemani.

Pili, mkazi mmoja wa ukoo wa Basimba kutoka Karagwe, anadai kuona stakabadhi ya kodi ya mwaka 1912 iliyolipwa na baba yake miaka michache baada ya kuhamia. Naye anakumbuka baba yake akizitaja familia nne alizozikuta sawa na zilizotajwa hapo juu. Hii inamaanisha Basimba kutoka Karagwe wameingia Nyakatoke kwenye miaka ya 1910. Mzee wa kwanza wa Basimba (toka Karagwe) kuja Nyakatoke, mzee

Mulokozi Kyaruzi Kairukabi, alikaa karibu na ulipo uwanja wa mpira karibu na pori, kwani alitegemea sana uwindaji katika maisha yake. Yaelekea mapori yalikuwa bado yana wanyama wengi na uwindaji ulikuwa ni shughuli ya uzalishaji wala siyo spoti kama ilivyo leo, kwani mfanya biashara wa nyama kutoka Kikomero, Mzee Muchuruza, anadai alipata shida sana kuuza nyama yake siku ambazo wawindaji walipata mawindo mazuri.

Kati ya koo zilizofuatia kuja Nyakatoke ni Bahimba. Hawakumbuki kwa uhakika ni lini Mzee wao, Kalisa baba yake na Kamukama alikuja Nyakatoke, lakini ushahidi unaonyesha kuwa alikuja kati ya mwaka 1910 na 1920, kwani haorodheshwi katika familia zile nne zilizokuwepo 1910, na Mzee Tibihika (Muhunga) aliyezaliwa Nyakatoke kwenye 1920 muda mfupi baada ya wazazi wake kuhamia, anadai kuwa baba yake (Kabwebwe) alihamia kutoka Karagwe kwa kukaribishwa na Kamukama Kalisa ambaye alikuwa rafiki wa damu (*munywanyi*[16]). Kalisa inadaiwa alikuja kwa shughuli za biashara kutokea Bugandika-Kiziba, na baadaye kuamua

---

[16] ***Munywanyi*** *(uw.banywanyi*)- rafiki wa damu. Urafiki huu ulifanyika kwa kuchanjana kwenye vitovu, kupaka damu ya kila mmoja kwenye punje ya kahawa, na kila mmoja kula punje yenye damu ya mwenzake. Baada ya hapo, wawili hao walihesabika sawa na ndugu wa kuzaliwa.

kuishi. Jamaa zake wameendelea kuhamia kwa kumfuata hadi miaka ya 1970.

Kulingana na ushahidi huo, Bahunga kutoka Karagwe, yaani familia ya sasa ya Tibihika, walihamia baada ya Bahimba wa familia ya Kamukama.

Kati ya wazee, yanaongelewa majina mengine mawili ambayo yanaweza kumaanisha makazi ya awali kabla ya familia nne zilizotajwa mwanzo. Kwanza mkazi mmoja wa ukoo wa Bayango kutoka Biharamulo (tarehe za kuja kwao hajijulikani) anakumbuka kusikia akiiongelewa *muharambwa* [17]aliyewahi kuishi Kibale kya mulimi, maeneo yalipo mashamba ya Agrimina na Mzee Saulo Bulowa. Kwa kuwa kiutamaduni *muharambwa* ni mtu aliyekuwa na jukumu la kusimamia ardhi za *mukama* [18]zilizotumiwa na raia kwa mazao ya muda, na inasemekana kawaida aliteuliwa kutoka koo za kawaida za wakazi wa awali, ni dhahiri kuwa aliishi hapa kabla au enzi za familia zile nne. Kwa bahati

---

[17] ***Muharambwa*** (uw. *baharambwa*)-Katika utawala wa jadi ni mtu aliye kuwa na jukumu la kusimamia ugawaji wa ardhi zilizokuwa chini ya mukama (hasa rweya) katika eneo lake, pamoja na kubariki zana za kilimo wakati wa msimu.

[18] ***Mukama*** (uw. *bakama*)- Mtawala wa jadi katika mojawapo ya falme saba za Bukoba na Karagwe. Wengine humwita chifu, lakini madaraka yake yalikuwa ni ya kifalme.

mbaya hakuna kumbukumbu zozote za jina wala ukoo wake.

Pili, kuna kitongoji kuitwa "Nyakatoke ka Mujunangoma". Haijulikani kama Mujunangoma aliishi Nyakatoke, lakini hapana shaka kuwa ndiye aliyeipa Nyakatoke jina au ambaye iliitwa hivyo kwa heshima yake. Kama aliwahi kuishi hapa basi aweza kuwa ndiye mwanzilishi. Lakini hatuwezi kusema hivyo kwa uhakika kamili, maana inasemekana kwamba wawindaji huwa na tabia za kuzipa majina sehemu mbali mbali porini ili kurahisisha safari zao za kuwinda. Kama sehemu hizi zikikaliwa na watu baadaye, hubakia na majina yake ya awali.

## 5.2. Kukua kwa Nyakatoke

Kufikia mwaka 1930, jumuiya ya Nyakatoke ilikuwa imefikia kaya zaidi ya kumi na mbili. Mzee Tibihika (1920), anaweza kukumbuka tisa, majina ya wakuu wa kaya hizo yamerodheshwa na koo zao katika mambano: Kalisa (Bahimba), Kabwebwe (Bahunga), Ruharara (Baziba), Ngambeki (Baziba), Matundwe (Bahunga), Kyaibale (Bahimba), Byabachwezi (Basimba), Rwenduuru (Bahunga) na Mulokozi (Basimba).

Kufikia enzi za utawala wa *Mukama* Kalemera (1916-1943) jumuiya ya Nyakatoke ilikuwa imekua, kufikia *Mukama* kumtuma Karagano

(familia ya sasa ya Mpira) kutoka Muhutwe aje kutawala Nyakatoke kama *mukungu*[19], Magenyi akiwa *mubezi* [20]wake. Hizi zilikuwa enzi za Kweyamba (kutoka Kanazi) akiwa Omwami wa Gombolora Kabirizi.

Hivi sasa, Nyakatoke inakaliwa na watu kutoka sehemu mbali mbali. Kuna familia nyingi kutoka Kiziba(kaskazini mwa wilaya ya Bukoba vijijini). Hawa walihamia hasa kwa kufuata mkondo wa karne nyingi wa kuelekea kusini wakisaka ardhi yenye rutuba, wakitokea kwenye maeneo yenye wakazi wengi ambako ardhi imechoka, na ambapo mashamba yamemegwa kiasi cha kutokidhi mahitaji.

Baadhi ya wakazi wa sasa wametoka Karagwe wakielekea mashariki. Hawa bila shaka hawakuwa wakitafuta ardhi, kwani ardhi Karagwe ilikuwa nyingi na bora kuliko ya Bukoba.

Tofauti na vijiji jirani, Nyakatoke imekuwa tofauti kwa kuwa na wahamiaji wachache sana kutoka Kiamutwara (Bukoba Vijijini mashariki), ambako hali ya ardhi na makazi ingetarajiwa

---

[19] ***Mukungu*** (uw. *bakungu*)- Mtawala wa kijiji au vijiji kadhaa aliyeteuliwa na mukama.

[20] ***Mubezi*** (uw. *babezi*)- Mtawala wa jadi aliyekuwa chini ya mukungu . Aliongoza sehemu ya kijiji.

kusababisha uhamiaji kuja hapa. Kwa kuwa vijiji na vitongoji jirani vina familia nyingi tokea maeneo hayo, ingefurahisha kujua ni kwa nini Nyakatoke ikawa tofauti.

Baadhi ya familia zimehamia kutoka Kihanja na Ihangiro (Nyada za Juu za Muleba). Sababu zinaelekea kuwa uhaba wa ardhi, lakini haijulikani kwa nini wamechagua maeneo haya, kwani sehemu za karibu zilizo kusini mwa Muleba pia zingewafaa.

Kumekuwepo pia wahamiaji kutoka nchi jirani za Rwanda na Burundi. Baadhi walikuwa wachungaji waliofuata maeneo ya malisho kwa mifugo yao, wakati wengine walikuja kama wafanyakazi wa mashambani na wachungaji wa mifugo kwenye nusu ya kwanza ya karne ya ishirini, na baadaye kuamua kuishi. Kundi hili limezidi kuongezeka shauri ya wakimbizi wa vita visivyoisha katika nchi zao kuanzia miaka ya 1960.

Wimbi la mwisho la wahamiaji lilikuwa ni la watu wenye asili ya Rwanda (hasa wafugaji wa Kitutsi) walioikimbia Uganda enzi za Fashisti Idd Amin, ambako walikuwa wakiishi kama wakimbizi. Walipewa ardhi kusini-magharibi mwa Nyakatoke, upande wa pili wa barabara itokayo Rubale kuelekea Burigi, ambapo mbuga ilikuwa wazi kwa malisho. Kufuatia Watutsi kuchukua tena madaraka Rwanda 1994, wengi

wao waliamua kurejea kwao, zikibakia familia chache tu. Tofauti na wengi wanavyofikiri, kitongoji cha Nyakaaro hakikupewa jina hilo kutokana na *balaaro* [21]hao kuishi hapo, bali kiliitwa hivyo baaada ya *Mukama* of Kihanja kupiga kambi hapo, kwenye eneo ambako sasa ni mashamba ya Mustafa na Barambirwa.

## 5.3. Muundo wa Makazi

Makazi ya muda mrefu yako karibu na mto na kusini mwake. Bado kuna kuhamahama sehemu za kusini magharibi penye wahamiaji wengi wapya ambapo ardhi si nzuri sana, na magharibi mwa barabara kwenye maeneo ambayo hapo awali yalikaliwa na *balaaro*. Vivyo hivyo makazi bora yako katikati ya kitongoji, wakati wahamiaji wapya wamo katika harakati za kujijenga nao wafanane na wakazi wa zamani. Wakazi walio wengi wako kati ya mto na maeneo mapya upande wa kusini. Haina budi kuzingatiwa kuwa kadri muda unavyopita mashamba mengi yamebadilika wakaaji, hivyo baadhi ya mashamba ya kihistoria hivi sasa yako mikononi mwa wakazi wapya.

---

[21] ***Balaaro*** (um. *mulaaro*)-Watu wa jamii ya Kihima wanaoishi kwa kufuga ng’ombe. Huhamahama kufuata upatikanaji wa malisho ya mifugo yao, ingawa wengi siku hizi huwa na makao ambayo kwa kiasi fulani ni ya kudumu.

Nyingi za familia za awali zitakuwa zilihamia hapa kabla ya kufuata imani na dini za kisasa. Walikuwa bado ni wafuasi wa imani za asili, zilizozingatia ibada za *Bachwezi* [22]na *Bazimu*[23]. Mhamiaji mpya alikuja na mbegu au mche wa mti (bila shaka kutoka kwenye *kigabiro* [24]cha ukoo wake) kama mwendelezo wa imani, ambao aliupanda kwenye makazi yake mapya. Boma la *biramula* [25]lilizungushiwa mti huu, nao ukawa madhabahu (*ekigabiro)* ya ibada na kafara kwa mizimu na mababu. Muda si muda walianza kuabudu kwa dini mpya hasa Ukristo na Uislaamu. Kwa bahati mbaya, tofauti na jumuiya zenye umri mkubwa zaidi, watu walibadili dini wakati *bigabiro* vikingali vidogo, hivyo kutunyima kigezo muhimu cha kukadiria umri wa wakazi.

---

[22] ***Bachwezi*** (um. *muchwezi*)- Miungu wanaoaminika kuwa walikuwa wa ukoo wa watawala wa zamani au watu mashuhuri katika maeneo ya maziwa makuu.

[23] ***Bazimu*** (um. *muzimu*)- Mizuka ya mababu katika ukoo.

[24] ***Kigabiro*** (uw. *bigabiro*)- Mti uliotumika kama madhabahu katika imani ya asili ya Wahaya, palipofanyikia ibada na sadaka kwa Bachwezi na Bazimu.

[25] ***Biramula*** (um. *kiramula*)- Mimea inayotumika sana kama mipaka ya ardhi Buhayani.

## 5.4. Mustakabali wa Jamii

Wakati dunia inaingia millenia mpya, Nyakatoke ni jumuiya mchanganyiko yenye kaya 120 hivi, ikiwa na jumla ya wakazi 600, ambapo 286 ni wanaume, 314 ni wanawake na 346 ni watoto walio chini ya miaka 18. Kaya zimegawanyika katika koo zaidi ya 29 zenye watu kutoka karibu pande zote za mkoa wa Kagera na nje yake. Hali hii ya mchanganyiko, ikijumuishwa na hali ya kutokuwepo kundi moja lenye nguvu (ukoo mkubwa kuliko zote una jumla ya kaya 23ambazo ni 19.3% ya kaya zote za kitongoji), inapunguza hisia na migongano za wakazi wake. Hali hii inawezesha kuwepo kwa jumuiya huru, wazi, yenye kuvumiliana, yenye ushirikiano mkubwa na isiyo na matabaka kama ilivyo Nyakatoke leo.

**JEDWALI 5: Wakazi wa Nyakatoke**

| Umri (miaka) | JINSIA | | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | ME | KE | |
| Chini ya 10 | 93<br>15.5% | 104<br>17.3% | 197<br>32.8% |
| 10 – 20 | 75<br>12.5% | 74<br>12.3% | 149<br>24.8% |
| 20 – 30 | 38<br>6.3% | 50<br>8.3% | 88<br>14.7% |
| 30 – 40 | 29<br>4.8% | 29<br>4.8% | 58<br>9.7% |
| 40 – 50 | 22<br>3.7% | 23<br>3.8% | 45<br>7.5% |
| 50 – 60 | 14<br>2.3% | 14<br>2.3% | 28<br>4.7% |
| 60 – 70 | 9<br>1.5% | 7<br>1.2% | 16<br>2.7% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 70 – 80 | 3<br>.5% | 8<br>1.3% | 11<br>1.8% |
| Zaidi ya 80 | 3<br>.5% | 5<br>.8% | 8<br>1.3% |
| JUMLA | 286<br>47.7% | 314<br>52.3% | 600<br>100.0% |

Takwimu hizi zimekusanywa na utafiti huu Februari 2000

Mhamiaji mgeni inaelekea anakubalika katika jumuiya kwa urahisi na haraka. Familia mbili ambazo zimehamia hivi karibuni wanashuhudia hili: Familia ya kwanza, kutoka Bugabo (kaskazini mashariki mwa wilaya ya Bukoba Vijijini), wanasema walijisikia kukubalika kabisa kijijini miezi sita tu baada ya kuhamia. Familia ya pili, kutoka Buganguzi (kusini magharibi mwa Wilaya Muleba), wanakiri walijisikia nyumbani miezi minne tu baada ya kuja Nyakatoke.

**JEDWALI 6: Koo za Nyakatoke**

| Ukoo | Idadi ya Kaya | Asilimia ya Jumla |
|---|---|---|
| BAYANGO | 23 | 19.3 |
| BASIMBA | 20 | 16.8 |
| BAHIMBA | 12 | 10.1 |
| BAHUNGA | 10 | 8.4 |
| BASITA | 9 | 7.6 |
| BAYOZI | 8 | 6.7 |
| BAMIRU | 6 | 5 |
| BAYEGO | 3 | 2.5 |
| BASINGO | 4 | 3.4 |
| BAGAYA | 3 | 2.5 |
| BAZIBA | 2 | 1.7 |
| BASHASHA | 2 | 1.7 |
| BATUNDU | 2 | 1.7 |
| BAJUBU | 2 | 1.7 |
| BARWANI | 2 | 1.7 |
| BALAMA | 1 | 0.8 |

| | | |
|---|---|---|
| BAGARA | 1 | 0.8 |
| BAKIREMBO | 1 | 0.8 |
| BAKOMBE | 1 | 0.8 |
| BASINDI | 1 | 0.8 |
| BAIHUZI | 1 | 0.8 |
| BAGWE | 1 | 0.8 |
| BAKURWA | 1 | 0.8 |
| BAHIRIRI | 1 | 0.8 |
| BAZIGABA | 1 | 0.8 |
| BALENGE | 1 | 0.8 |
| JUMLA | 119 | 100 |

Takwimu hizi zimekusanywa na utafiti huu Februari 2000

## 6. UHAKIKA WA JAMII KATIKA KUKABILIANA NA 'MAZINGIRA' (MAISHA YA KILA SIKU)

### 6.1. Ushirikiano: zamani na sasa.

Inakubalika kuwa zamani chakula kilikuwa kingi na maisha yalikuwa rahisi kiasi cha kuruhusu utaratibu wa kawaida wa mahusiano. Majirani, ndugu na marafiki walishirikiana kikamilifu na bure wakati wa raha na masikitiko kama vile harusi, kuzaa, kuuguza na msiba. Walishirikiana kazi zao kwenye shughuli mbali mbali kama vile ujenzi wa makazi yao, uchungaji, uvuvi na uwindaji. Walihudhuria kwenye matukio ya dhalura kama vile, kuungua kwa nyumba, kuvamiwa na majambazi au wanyama pori.

Kufuatia kufifia kwa uzalishaji na msukumo wa maisha ya kisasa wa kuingia kwenye uchumi wa kifedha, taratibu na mipangilio ya kushirikiana ilibadirishwa na kuiga yaliyo mema ili kuweza

kuishi. Michango ilipaswa kusimamiwa kiuhakika, mahudhurio kurekodiwa, sheria kuandikwa, akiba kutunzwa na majukumu ya viongozi na wanavikundi kufafanuliwa waziwazi. Hii ilipelekea kuzaliwa kwa taratibu mathubuti katika ushirikiano mpya ambao unafaa sehemu ya maisha ya kila siku ya walio wengi katika Nyakatoke ya leo.

Nyakatoke imepitia hatua nyingi na mbali mbali za mifumo ya ushirikiano wa kipekee. Haya yalikuwa ni matokeo ya mifumo tofautitofauti. Katika jamii hii kuna vikundi vya kina mama, kina baba na baadhi mchanganyiko. Hivi husaidiana kwenye misiba, kuuguza, kupongezana (*kwihukya*[26]*)* kwa tukio maalum au bila tukio ili mradi ni zamu ya mwanakikundi, kushirikiana kazini, kuchangiana kwa mzunguko na kulindana kiroho. Pia kutunza akiba ya mwanakikundi binafsi au kikundi chote kwa pamoja na ushirikiano kiuzalishaji mali.

## 6.2. Muungano na Bujuni

Vikundi vikubwa na vyenye nguvu ni Muungano na Bujuni ambapo, Muungano huundwa na

---

[26] ***Kwihukya***- Kupongeza. Hutumika kwa maana ya kumpongeza mtu kwa tukio la raha kama kupata mtoto, kufunga ndoa, n.k. Hii inaweza kuandamana na zawadi. Katika Nyakatoke kwihukya hufanyika rasmi kwa kundi kumletea mhusika zawadi mbali mbali kwenye tafrija fupi.

karibia wanawake wote kupitia vyama vyao vidogovidogo saba; na Bujuni ambacho kinaundwa na karibia kaya zote katika jamii hii inayounganisha na baadhi ya kaya toka kitongoji cha jirani Nyakalaaro. Hiki kikundi kinahusisha wakuu wa kaya. Wakuu hawa waliowengi ni wanaume na wanawake kidogo. Pia, watoto wadogo wanawakilishwa kama wanakikundi iwapo ni wakuu wa kaya zao.

Kujiunga na vikundi hivi bado ni hiari kukisisitizwa na woga wa kutokusaidiwa unapokuwa mhitaji. Sifa za kupokelewa na Bujuni yakubidi uwe na kaya (hili halifuatiliwi sana) na Muungano yabidi kaya atokamo mwombaji iwe mwanachama wa kikundi cha Bujuni.

Vikundi hivi hubeba jukumu la kusaidiana (bima) katika jamii hii. Muungano husaidia kwenye misiba na magonjwa kulingana na katiba yao. Bujuni nayo husaidia msibani pekee; misiba hii lazima ifanyike kijijini ikiwa ni pamoja na mazishi. Ni kwa uhusiano gani wanasaidia, hili inaelezwa kwenye katiba.

Vikundi saba vya Muungano, hukirahisisishia kikundi hiki kazi (usimamizi) ya kuwa na kundi kubwa la wanachama. Vikundi hivi, vingine havifanyi lolote zaidi ya kuwapa wanachama wake vibali vya kuingilia Muungano. Vikundi vingine vina shughuli nyingi nje ya Muungano.

Vikundi hivi hupongezana (*kwihukya*) husaidiana kwenye harusi, sherehe na tafrija. Pia huongezea michango mingine kwenye vifo na magonjwa juu ya ile watoayo katika Muungano. Aidha hutunziana akiba za binafsi au za jumla zipatikanazo kwa kufanyiana vibarua mashambani. Pia husaidiana kazi zao.

## 6.3. Vikundi vingine

Vikundi vingine vina mchanganyiko wa wanachama kutoka ndani na nje ya jamii hii (mf. Chama cha Kusaidiana na Maendeleo, m/k Leopord). Kama dhana ya vikundi vingine ilivyo hivi pia husaidiana kwenye misiba na uuguzi. Pia hutunza akiba ya wote (jumla) na wanachama hufaidika kwa kuchukua mikopo toka mfuko wao.Vingine hujiendesha kama uwekezaji (ushirika) mdogo kwa kufuga, kulima na mipango ya kuweka vitega uchumi kv. Kinu cha kusagia nafaka.

Utafiti pia umeona kuwa Nyakatoke, kama jamii nyingine, ni vigumu kwa mtu binafsi kujiwekea akiba bila msukumo wa pembeni. Hivyo wanajamii walifikiria mpango wa kuchangiana katika vikundi (*ROSCA*[27]) ambapo mtu hutoa kidogo kidogo na kupokea kitita cha hela kwa

---

[27] **ROSCA** – Kifupi cha maneno ya Kiingereza yanayomaanisha kuchangiana na kutunziana pesa kwa zamu.

pamoja. Vikundi hivi vinatimiza jumla ya 40 ambayo ukilinganisha na ukubwa wa Nyakatoke si idadi mbaya iwapo watu wanavitumia. Aidha katika vikundi hivi wahusika huchangiana katika mpangilio maalum waliokubaliana wa kuzungukiana kwa kupeana kiasi maalum. Wengine hupeana kiasi awezacho mtu ili mradi atarudishiwa kiasi hicho hicho toka kwa mchangiwaji. Vipo vikundi vya vijana, wanawake na vile vya kidini ambavyo hujumuisha wote. Vingi vya vikundi hivi huchangiana mara moja kwa mwezi.

Katika Nyakatoke walio wengi ni waumini katika madhehebu mbalimbali japokuwa hakuna sehemu maalum za kuabudia katika Nyakatoke. Wahusika wa jamii hii wamejihimu ama kuuda au kujiunga katika vikundi vya kidini. Mbali na kazi ya kulindana kiroho pia husaidiana kijamii na kiuchumi katika baadhi ya vikundi hivi, wahusika husaidiana wawapo na tafrija au hafla mbalimbali zinazokubalika katika kikundi husika, pia wauguapo na kuuguza au wanapokumbwa na misiba ama kufa wenyewe. Vikundi tunavyojua mpaka sasa ni vile vya Kiislam, Kikatoliki na Kilutheri ambavyo vinatimiza idadi ya vikundi vitano.

Kusaidiana katika kazi hakukusahaulika katika jamii hii; wanawake kwa mfano hulima au kupalilia mashamba yao katika vukundi kwa kuzungukiana mmoja baada ya mwingine. Pia

itokeapo mmoja wao akawa na upungufu na uhitaji wa nguvu ya ziada kwa sababu zinazokubalika, basi hupewa nguvu hiyo.Vikundi hivi si vyote vilivyo kwishajiwekea utaratibu wa wazi, vingi vyao huwa ni sehemu ya vikundi vya akinamama (*luhaaso*[28]), majirani, watu wa ukoo ama familia zilizo karibu. Vikundi tunavyoweza kuviita vya wanaume ni vile vya wafugaji wanaochunga pamoja kwa mzunguko katika utaratibu uliowekwa wazi vikiitwa *buyo*[29], ambapo mtu huchunga siku mbili mfurulizo kabla ya wenzake pasipokujali ukubwa au idadi ya mifugo yake. Kuna *mayo* matatu katika jamii hii, ambapo kundi moja tu ndilo linahusisha watu wa Nyakatoke pekee.

Katika kukabiliana na maisha watu wa jamii hii wameanzisha ushirikiano wa kutunziana akiba. Akiba hizi nyingine hutumika kama vitega uchumi na nyingi ni kutunza uwezacho tu. Katika vitega uchumi hivi wahusika hulima

---

[28] ***Luhaaso*** (uw. *mpaaso*)- Neno linalomaanisha kifaa cha kumenyea ndizi kilichotengenezwa kutokana na mwanzi. Hapa lina maana ya vikundi vya kina mama ambavyo awali lilitokana na kusaidiana kumenya ndizi na kupika kwenye sherehe na vilio.

[29] ***Buyo*** (uw. *mayo*)- Kundi la ng’ombe wa familia mbali mbali wanaochanganywa pamoja ili kurahisisha shughuli ya uchungaji. Kila siku mifugo hukusanywa pamoja asubuhi na kuchukuliwa na wenyewe jioni. Kazi ya kuchunga hufanyika kwa zamu kati ya familia husika.

mazao kwa pamoja ama kufuga kwa pamoja (mifugo k.v. nguruwe na mbuzi) kwa mipango ya kugawana ziada tu. Mpango wa kutunziana akiba umo ndani ya vikundi vya akina mama (*luhaaso*) japo si kwa wote. Kina mama hawa hufanya kazi mashambani kwa kulipwa (*kigodi*[30]) ambapo pia malipo hutofautiana kati ya mwanakikundi na asiye mwanakikundi. Kawaida *muzizi* [31]mmoja utolewao na mtu mmoja hulipiwa sh.200. Lakini kulingana na taratibu za kusaidiana katika vikundi, mwanakikundi hulipa sh.150 kwa kila *muzizi*. *Mizizi* yote afanyayo mhusika inahesabiwa na malipo yake hutunzwa na mgawanyo hufanyika mwishoni mwa mwaka kwa kuzingatia kuwa muhusika anavuna alichopanda.

## 6.4. Ushirikiano nje ya Makundi

Mbali na makundi haya, watu husaidiana mtu na mwenzie kama jadi ilivyo. Watu husaidiana kwenye shughuli zao za kila siku na kupeana mkono kwa lolote geni linalowasibu. Wagonjwa hupelekwa hospitali, wafu huzikwa na wafiwa kufarijiwa. Aidha mioto itokeapo huzimwa na mikopo mikubwa kwa midogo inaendelea. Pia zawadi hutolewa na mambo mengine mengi ya kiutu. Kweli Nyakatoke ni mfano bora wa ushirikiano (wa kuigwa) kama kibwagizo kimojawapo cha nyimbo za kinamama kisemawavyo,

---

[30] ***Kigodi***- Neno linalotumika sana maeneo haya kumaanisha kazi ya kibarua, hasa hasa cha shambani.

[31] Muzizi (uw. mizizi)- Muda wa kufanya kazi mfululizo, kwa wastani masaa matano. Kipimo hiki hutumika

kikiwaita wasioshirikiana waje waone: *ayang'Obumo naij'Alore*.

**Ambatisho: Ramani ya Mgawanyo wa Mvua katika Wilaya za Bukoba na Muleba.**

